JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA TATU

Marchi 2024

Rais Samia Awataka watanzania kuyaishi maisha ya Hayati Mwinyi

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.

www.pmo.go.tz

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Watanzania tuna wajibu wa kuendelea kustahimiliana na kufanya siasa za kistaarabu zinazoweka mbele maslahi ya nchi.

Rais Samia amesema hayo wakati wa ibada ya mazishi ya aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa yaliyofanyika katika kijiji cha Ngarash wilayani Monduli.

Aidha, Rais Samia amesema njia pekee ya kumuenzi Hayati Lowassa ni kuendesha siasa

Aidha, Rais Samia amesema kwa ustahamilivu wake wakati wa uongozi, hayati Mwinyi aliheshimu haki za binadamu na utawala bora na kuruhusu maoni tofauti yenye kuikosoa serikali. Vile vile, Rais Samia amesema licha ya Hayati Mwinyi kuwa kiongozi katika vipindi vigumu kisiasa na kiuchumi aliweza kuhakikisha utulivu na kufanya mageuzi makubwa katika nyanja za kisiasa na kiuchumi.

Rais Samia pia amesema Hayati Mwinyi ana mchango endelevu uliozisaidia serikali za awamu zilizofuatia kwani ndiye aliyehamasisha uwekezaji kutoka sekta binafsi na soko huria zilizochangia katika ukusanyaji mapato. Kwa upande mwingine, Rais Samia amewataka Watanzania kuishi kwa kufuata misingi bora ya maisha na malezi na kuyachukulia maisha ya Hayati Mwinyi kama funzo katika kuwalea vijana kwa kuzingatia maadili ya dini na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Hayati Mwinyi ameacha alama za kudumu na za kihistoria kama Rais wa mwisho kuiongoza Tanzania katika mfumo wa chama kimoja na kuweka ukomo wa mihula ya Urais.

Waziri Mhagama Awataka watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuendelea kutekeleza majukumu kwa ubunifu

Waziri Wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera,Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama ametoa wito kwa Baraza la Wafanyakaziwa Ofisi hiyo,kupitia taarifa ya utekelezaji wa bajetiya mwaka 2023/24 na makadirio ya bajeti ya mwaka 2024/25.

kwa umakini ili kuona yale yaliyotekelezwa kwa mwaka uliopita wa fedha na kuongeza ubunifu utakaowezesha rasilimali kidogo zilizotengwa kuleta matokeo makubwa zaidi kwa mwaka ujao wa fedha.

Amesema kwa kufanya hivyo wataisaidia Ofisi hiyo kufikia malengo na watamwezesha kila mtumishi kuwajibika ipasavyo na kwa weledi ili kupata mafanikio ya pamoja.

Mhe. Mhagama ametoa kauli hiyo leo Machi Jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)

Mhagama amewataka wajumbe wa Baraza hilo kuwa huru katika majadiliano hasa wakati wa agenda

kuu ya kupitia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 na makadirio ya bajeti ya mwaka 2024/25 na kwa umakini ili kuona yale yaliyotekelezwa kwa mwaka uliopita wa fedha na kuongeza ubunifu utakaowezesha rasilimali kidogo zilizotengwa kuleta matokeo makubwa zaidi kwa mwaka ujao wa fedha.

" Kujadili bajeti ya Ofisi ni mojawapo ya majukumu ya msingi ya Baraza na yameainishwa katika mkataba unaounda Baraza hili na hii ni muhimu kwa mustakabali wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi, naamini nyote mnafahamu namna tunavyoshiriki kwa pamoja katika maandalizi ya bajeti ya Ofusi ya Waziri Mkuu kila mwaka wa fedha ili kupata zizazokidhi mahitaji ya ofisi pamoja na utekelezaji wa majukumu tuliyopewa na Rais kupitia hati idhini iliyoanzisha ofisi hii," amesema Waziri Mhagama.

Pia amewasisitiza kufanya kazi kwa umoja, ushirikiano, bidii, weledi na kuendeleza utamaduni wa kukutana kwa lengo la kuboresha utendaji kazi kwa manufaa ya Taifa.

Pia amewaomba watumishi hao kutumia muda wao wa kazi vizuri ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu waliyopewa kwa ufanisi na kujituma ili kufanya kazi kwa viwango vya juu na kufikia malengo yaliyowekwa na ofisi pamoja na kutimiza ndoto zao binafsi katika utumishi.

"Msiweke matabaka na jitahidini kuepukana na migongano na migogoro mahali pa kazi ili kuleta tijja na upande wa menejimenti nawahimiza kusimamia ipasavyo utendaji wa wafanyakazi na upatikanaji wa haki na maslahi yao," amesisitiza Mhagama

.

.

Waziri Mhagama akabidhi Magari na Pikipiki zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa Watekelezaji wa Programu ya AFDP

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama amekabidhi vifaa vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni Mbili za kitanzania kwa watekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP).

Akikabidhi vifaa hivyo ambavyo ni Magari, pikipikiza miguu miwili na mitatu (guta) kwa wawakilishi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo, Wakala wa Mbegu (ASA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Taasisi za Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSCI) na Mratibu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uraibu).

Waziri Mhagama alieleza kuwa upatikanaji wa vifaa vinavyonunuliwa kupitia Programu hiyo ikiwemo magari na pikipiki, ni vitendea kazi muhimu katika utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 bahari kuu na kuendeleza ukuzaji viumbe maji, na kilimo cha Mwani.

"Vilevile, Programu hii inalenga kuongeza uzalishaji, tija na faida katika shughuli za wakulima kwa kuendeleza shughuli za ugunduzi na uzalishaji wa mbegu bora na kuhamasisha kilimo cha mazao lishe (nutritional sensitive) ili kupunguza udumavu." Alifafanua Waziri Mhagama

Aliendelea kusema kuwa Programu hiyo inaenda kuleta mabadiliko makubwa kwenye uzalishaji na uendelezaji wa biashara kwa kuzingatia mazingira halisi yaliyopo na hasa uboreshaji wa uzalishaji wa mbegu za mazao ya kilimo, mahindi, alizeti, maharage na mimea jamii ya kunde pamoja na uboreshaji wa sekta ya uvuvi, mifugo na ufugaji wa viumbe maji kwa lengo la kuwaendeleza na kuwawezesha akina mama na vijana wa kitanzania

kunufaika zaidi na sekta hizo mbili.

Akizungumza kwa Niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar) Mheshimiwa Hamza Hassan Juma alisema matunda ya mafanikio haya ni matokeo ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioasisiwa na Hayati Baba wa Taifa Mw. Julius Kambarage Nyerere na Hayati Shekhe Abeid Amani Karume takribani miaka sitini iliyopita, "kwenye zoezi hili kuna kipengele cha ununuzi wa meli za uvuvi ambazo tutazipata sisi kutokana na faida ya Muungano wetu." Alibainisha

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde alisema vifaa hivyo vitaenda kuchochea kasi ya utekelezaji katika sekta ya kilimo hasa katika shughuli mbalimbali zilizopangwa katika utekelejazi wa program hiyo na kutoa rai kwa taasisi zote zilizo chini ya Wizara hiyo zinahakikisha vifaa hivyo vinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuweza kufikia malengo ya Programu.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria yapitisha makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2024/25.unifu

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25 ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo.

Hayo yamesemwa na Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Florent Laurent Kyombe akikaimu nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo hii leo katika Ofisi za Bunge Jijini Dodoma mara baada ya wajumbe kujadili na kuridhia bajeti katika Ofisi za Bunge Jijini Dodoma mara baada ya wajumbe kujadili na kuridhia bajeti katika kikao kilichohusisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo, wataalamu kutoka Idara na Vitengo vya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Alieleza kuwa bajeti ya ofisi hiyo iwe yenye matokeo changa na kusaidia kuleta maendeleo kwa wananchi

huku akiipongeza Ofisi kwa kazi kubwa ya uratibu wa Shughuli za Serikali.

"Kipekee Kamati imepitisha makadirio ya bajeti hii muhimu mara baada ya kusikia wasilisho na kujadili kwa kina, tunashukuru kwa wasilisho endeleeni na jukumu la uratibu wa shughuli za Serikali kwa manufaa ya jamii katika kujiletea maendeleo," alisema Makamu Mwenyekiti huyo.

Awali akiwasilisha taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25 mbele ya kamati hiyo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama ameishukuru kamati kwa kujadili na kupitisha makadiri ya bajeti hiyo huku akisema Ofisi yake itaendelea kufanya kazi kwa weledi zaidi kwa kuzingatia jukumu la msingi la Uratibu wa Shughuli zote za Serikali.

Pia Waziri Mhagama alisema mpango wa shughuli zitakazotekelezwa kwa kutumia bajeti hiyo ya mwaka wa fedha ujao 2024/25 ambapo wanakamati kwa kauli moja walipitisha makadirio ya bajeti hiyo.

"Ni imani yangu kuwa bajeti hii itakapopita tunakwenda kutekeleza malengo yetu huku tukihakikisha shughuli mbalimbali ikiwemo za uratibu wa masuala ya maafa, uratibu wa shughuli za bunge, masuala ya tathmin na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali pamoja jukumu la uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba Dodoma unaendelea vizuri ikiwa ni moja ya majukumu katika kuratibu," Alisema Mhe. Mhagama

Akizungumza kuhusu masuala ya Ofisi ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali alihakikishia Kamati kuwa wataendelea kuboresha mitambo na kuisimamia vyema ili kuhakikisha kila nyaraka za Serikali ziendelee kuchapwa kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali.

Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI Yatembeela gereza la Chato

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imetembelea Gereza la Wilaya ya Chato kwa lengo la kujionea namna mwitikio wa UKIMWI unavyotekelezwa katika gereza hilo ambapo wamekutana na mahabusu, Wafungwa, Askari, Maafisa pamoja watumishi wa umma.

Akizungumza katika ziara hiyo mwishoni mwa wiki Mkoani Geita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI Mhe. Stanslaus Nyongo alisema kamati imeridhishwa na jinsi . Magereza inavyopanga na kutekeleza mikakati ya Mwitikio wa UKIMWI katika gereza hilo.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa afua za Mwitikio wa UKIMWI katika gereza la Chato zinaridhisha ambapo alimpongeza Mkuu wa Jeshi la Magereza kutokana na kuhakikisha wafungwa na mahabusu wanakuwa salama kiafya.

“Nitumie nafasi hii kumshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani kila kinachofanyika ni kutokana na mwongozo na maelekezo yake.

Pia niwasisitize kuchukua tahadhari ya maambukizi ya VVU ikiwa ni pamoja na kupima afya kwa wale ambao hawajapima ili mjue afya zenu, pamoja na kuanzishiwa dawa kwa wale ambao watagundulika kuwa na maambukizi ya VVU,"Alisema Mhe. Nyongo.

Vile vile aliiomba Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kuangalia namna ambavyo itaandaa mkakati maalum wa kutekeleza afua za UKIMWI katika magereza yote nchini ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo maafisa magereza katika utoaji elimu ya VVU katika maeneo yao.

"Niombe Ofisi ya Waziri Mkuu kama Mratibu wa masuala ya UKIMWI muangalie namna mtakavyo kuwa na mkakati wa kutekeleza afua za UKIMWI katika magereza nchini na kufanya magereza kuwa Mkoa wa kimkakati,ili kuhakikisha maambukizi ya VVU yanapungua pamoja na kuwawezesha Maafisa Magereza kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU,"Aliongeza.

Kwa upande wake Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Ummy Nderiananga alieleza kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inapokea maagizo yote yanayotolewa na Kamati hiyo kwa ajili ya Utekelezaji.

"Nilipongeze Jeshi la Magereza kwa kuendelea kutekeleza afua za Mwitikio wa UKIMWI pamoja na kuweka mikakati mizuri ambayo inalenga kumaliza UKIMWI ifikapo 2030,"Alipongeza Mhe. Nderiananga.

Kamati ilikutana na Mahabusu na Wafungwa ambapo katika risala yao wamebainisha changamoto zinazowakabili na baadhi ya changamoto zilipata utatuzi kutoka Machi kuisha uongozi wa Jeshi la Magereza ikiwa ni pamoja na kuwanunulia magodoro 50 kabla ya mwezi Machi kuisha , pamoja na kufanya utaratibu wa kuchimba kisima cha maji ili kupunguza changamoto ya maji.

Ilemela yakabidhiwa Mpango wa Usimamizi wa Maafa

SERIKALI imekabidhi nyaraka za usimamizi wa maafa katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela Jijini Mwanza huku ikisisitiza kuwa, ni muhimu masuala hayo kujumuishwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku siku ili kuendelea kuwa na matokea chanya katika masuala ya menejimenti ya maafa nchini.

Wito huo umetolewa Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu Brigedia Jenerali Hosea Ndagala akimwakilisha Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dkt. Jim Yonazi wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Nyaraka za Usimamizi wa Maafa katika halmashauri hiyo.

Nyaraka zilizokabidhiwa ni pamoja na za Matokeo ya tathmini ya vihatarishi, mpango wa kujiandaa na kukabiliana na maafa na mkakati wa kupunguza vihatarishi vya maafa nchini.

Brigedia Jenerali Ndagala ametoa wito kwa Idara, Vitengo na Taasisi zote zilizopo katika Halmashauri hiyo kuzingatia dira hii katika kutekeleza vipaumbele vya kisekta.

"Nitoe wito kwamba, nyaraka hizi zilizoandaliwa ziwe ni chachu ya kuongeza ushirikishwaji wa jamii na wadau, kujenga uelewa wa jamii kuhusu masuala ya usimamizi wa maafa,kuimarisha mfumo wa utoaji tahadhari ya awali, kujenga uwezo wa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa na kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa."alieleza

Amebainisha kuwa matokeo ya tathmini ya maafa iliyofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mwezi Februari, 2024 yameonesha kuwa Manispaa hiyo imekuwa ikikabiliwa na maafa.

Ameeleza kuwa maafa hayo yamekuwa yakisababishwa na majanga ya mafuriko, upepo mkali, moto, magonjwa ya mlipuko pamoja na ajali za barabarani na majini

Amesema anatambua kwa sasa Manispaa hiyo inakabiliwa na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu hivyo kuwapongeza kwa jitihada wanazoendelea nazo katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Aidha, amewasisitiza kuendelea kuchukua jitihada mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu.

"Ni imani yangu kuwa matokeo ya tathmini iliyofanyika yamezingatiwa ipasavyo katika kuandaa Mpango wa Kujiandaa na Kukabili Maafa na Mkakati wa Kupunguza Vihatarishi vya Maafa katika Manispaa ya Ilemela. Hivyo, ni matumaini yangu kuwa, mpango huu utasaidia sana kuongeza ufanisi katika kukabiliana na maafa kwa kuwa unaainisha majukumu ya wadau wote wanaohusika na masuala ya maafa katika Manispaa ya Ilelemela kabla, wakati na baada ya maafa kutokea. "amesema.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz